COMPETITION AUTHORITY OF KENYA

# KNOWLEDGE HUB

June 2026

Issue 17

## Miaka Thelathini na Sita Nyuma ya Usukani, Daima Mbele ya Barabara



***Bwana Joseph Njoroge -Dereva mstaafu wa CAK***

Hakuwahi kuwa kwenye habari za magazeti. Hakuwahi kuongoza mkutano wala kusaini sera. Lakini kwa miaka thelathini na sita, Bwana Njoroge alitokea kazini kwa wakati, tayari, amejipanga, na mwaminifu, kwanza katika Wizara ya Fedha, kisha katika Mamlaka ya Ushindani Kenya. Akistaafu sasa, mahojiano yake ya kuaga ni ukumbusho wa kimya kwamba ubora wa kitaalamu hauna cheo. Bwana Njoroge alitumikia serikali ya Kenya kwa utulivu na uaminifu kwa zaidi ya miaka thelathini. Anapostaafu, anaacha zaidi ya “logbook” safi - anaacha mfano wa heshima ya kitaalamu. Alistaafu kutoka CAK Juni, 2026.

| **36** | **25** | **~10** | **3** |
|---|---|---|---|
| Jumla ya miaka ya huduma | Miaka katika Wizara ya Fedha | Miaka katika CAK | Wakurugenzi/Makamishna aliotumikia |

**Tueleze kuhusu safari yako ya kazi kutoka wakati ulipojiunga na Wizara ya Fedha, hadi ulipojiunga na Mamlaka ya Ushindani?**

Kwa jumla, nimefanya kazi ya dereva kwa miaka thelathini na sita. Nimekua kazi pale katika wizara ya fedha kwa miaka ishiri na tano. Nimekua kwa Mamlaka ya Ushindani kwa miaka kama kumi na moja.

Kabla nianze kazi kama dereva wa mkurugenzi mkuu wa Mamlaka ya Ushindani, nilifanya kazi na kamishena wa kwanza katika wizara ya fedha. Kazi ilikua ngumu hapo mwanzo lakini nilifahamu kua ni muhimu kuongea, hivyo basi niliongea vyema na mkubwa na kazi ikawa sawa na nikafanya naye miaka saba kabla astaafu.

Baada ya hapo nikapewa mkubwa mwingine ambaye alikua kamishena pia na nikafanya naye kwa miaka saba kabla kujiuzulu kwake. Baada ya hapo, ndipo nikajiunga na aliye kua mkurugenzi wa kwanza wa mamlaka ya ushindani bwana Wang'ombe Kariuki ambaye nilifanya naye kwa miaka saba. Baada ya muda wake kuisha niliendelea na kazi ya huduma ya dereva kwa wafanyikazi wengine.

**Ni ushauri upi ambao unaweza wapa madereva wenzako wanapo pewa jukumu la kazi katika ofisi la mkurugenzi mkuu?**

Kitu cha muhimu ukitaka kukubalika katika hizo ofisi, cha kwanza ni usiwe mtu wa kuchelewa kazini, mkubwa akikuhitaji uwe mwepesi kupatikana. La pili, usiwe mtu wa uongo, usitoke bila kueleza mkubwa wako, eleza mkubwa wako iwapo hautapatikana baadaye.

Pia wajulishe wale wanaokupangia kazi kwa muda ufaao ili wapange kazi mapema. Lazima pia dereva afahamu kua anapaswa kujipanga na mahitaji yake kama ya chakula, sio kutegemea mkubwa wake wakati yuko kazi nje ya ofisi. La mwisho, unapoenda kwa mkubwa kikazi weka fahamu zako kwa kazi wala sio kuangalia tabia ya mkubwa.

**Wakati kuna shida barabarani kama maandamano, mafuriko ama mambo ya usalama kwa jumla, ni maarifa yapi ambayo ni muhimu kwa dereva kujua ili kumsaidia wakati kama huo**

Kunapokua na shida barabarani, kwa mfano kama maandamano, ni muhimu pia kujulisha mkubwa wako na kumueleza kama kuna haja ya kubadilisha njia ama kutulia hadi maandamano yaishe. Ni muhimu kwa dereva kujua barabara nyingi na tofauti sio kutegemea njia moja pekee.

Pia lazima dereva awe makini kujua kile kinachoendelea mjini ili ajulishe na kumshauri mkubwa wake mapema.

**Ni mawaidha yapi ya jinsi ya kufanya kazi vizuri ambayo unaweza mpa yule atakaye chukua nafasi yako wakati anapoenda kazi ya utafiti wa uwandani (fieldwork) na wenzake?**

Maafisa ndio wanaojua mahali ambapo wanaenda safari. Ni muhimu kuongea nao nakusikilizana jinsi mtakavyopanga njia kutoka mwanzo hadi mwisho. Kama dereva yafaa uwe na ufahamu mzuri wa barabara ndiposa uwe na uwezo wa kuelekeza wenzako.

La pili ni kwamba unafaa kueleza wenzako kwamba wakati mnafunga kazi pia gari inafaa kuelekezwa panapo faa ndio gari iwe salama hata nawe upate kupumzika na kujiandaa kwa siku inayofuata. Unafaa kufanya kazi vile ambavyo unaelekezwa na wenzako mukiwa uwandani. Pia ni muhimu kuendesha gari ukiwa hujalewa ili uweze kuaminika.

> *"Ukisimamishwa na polisi kwa kasi kupita kiasi, chukua wajibu wako. Usiweke lawama kwa mwenzako."*
>
> **— Bwana Njoroge — kuhusu uwajibikaji wa kitaalamu**

**Kwa sheria ambazo ziko za barabarani ama zinazohitajika kwa dereva hapa ofisini, ni yapi ambayo waweza sema yana faa kutiliwa maanani ama yarekebishwe?**

Sheria zilizowekwa hapa CAK ziko laini kabisa. Sheria ziko shwari na kazi hufanyika kwa haraka sana.

Kama dereva ni lazima ujue kujaza *workticket* inavyo faa. Unapokua barabarani na ushikwe na askari kwa sababu ya kuendesha gari kwa kasi yafaa uchukue wajibu na sio kuweka lawama kwa wenzako.

Unafaa uelewe sehemu za barabara ambazo hazitaki mwendo wa kasi ili usiwe na mvutano na askari barabarani. Lazima uwe mtulivu barabarani maanake watu huwa na tabia tofauti na unafaa uwe mfano mzuri hata kwa madereva wengine.

**Kwa muda ambao umekua CAK tueleze mfano mmoja wa nyakati nzuri ulipitia.**

Mimi hufarahia wakati kama dereva unaaminika hadi kiwango ambacho ofisi zingine za serikali pia zaweza kukuitisha kuwapa msaada. Hio huonyesha kwamba kazi yako ni nzuri na umeheshimika. Mwezi wa nne nilienda kwa muda katika ofisi ya mkaguzi mkuu was serilaki kuwapatia huduma wakiwa kwa kazi yao ya utafiti wa uwandani katika sehemu tofauti za nchi. Nilipokua huko nilifanya kazi yangu kwa ustadi na walifuria. Niliwakilisha CAK vyema.

**Je, kuna kitu chochote kiliwai kukushusha moyo wakati ulikua unafanya kazi yako hapa CAK?**

Sijafika kwa hicho kiwango, ningependa tu kusema ni vyema kuheshimu kazi yako. Kile ambacho CAK walipanga vyema ni kuhakikisha kwamba kila dereva yuko na gari lake na ni jukumu lake kulitunza vyema na kuhakikisha halina shida na pia linapelekwa kwa huduma ya gari kwa wakati unaofaa.

Kwa wale madereva watakaobaki ama kujiunga na CAK baadaye ni muhimu kuheshimu gari la mwenzako, usiwe mwepesi kuchukua gari ambalo mwenzako amepewa bila kumfahamisha, ili kuhakikisha gari zimechungwa vizuri na hakuna kulaumiana wakati jambo linapotokea.

**Kwa yule atakaye kuja baada yako, ni sehemu gani ya mafunzo unaweza mueleza atilie maanani?**

Ningesema mafunzo ya maana kwa dereva ni yeye mwenyewe kuchukua jukumu la kujifunza. Pia mafunzo ya kuendesha gari kwa tahadhari ni mafunzo ya muhimu haswa kwa dereva wa serikali.

**Tueleze kwa jumla umepanga kufanya nini baada ya kustaafu?**




Mpango wangu nikuenda nyumbani kupumzika na mke wangu. Jambo ambalo ningesema kwa wale ambao wanaelekea kustaafu ni kwamba wanapopata pesa ya malipo ya kustaafu wasiweke kwa biashara.

Maneno ya biashara ni mengi na kuna uwezekano kupoteza hela zako zote. Pia nitafanya ukulima kidogo wa mifugo kama kuku na mbuzi ili nipate chakula na matumizi ya hapo nyumbani.

Mungu amenijalia nimefanya kazi kwa miaka mingi na sasa ni wakati wangu kwenda kupumzika. Pia nafahamu kwamba sitakua na mshahara tena ila tu pesa ya kustaafu ambayo itakua chini kwa hivyo lazima pia nipunguze mahitaji yangu ili niweze kutosheka na kile nitakachopata.

**Ni mawaidha gani ya mwisho uliyonayo kwa familia ya CAK?**

Jambo muhimu zaidi ni kuheshimiana mahali pa kazi kuanzia mfanyakazi mkubwa hadi mdogo. Watu lazima wajifunze kufanya kazi pamoja bila dharau, hapo ndipo kazi itafanyika vizuri kweli kweli. Na anza kupanga kustaafu mapema ukiwa bado mchanga na una kipato cha kutosha. Usisubiri hadi karibu na wakati wa kuondoka.

## MAFUNZO YA KUKUMBUKA

- Kuaminika ni aina ya ubora. Kukua mwepesi wa kupatikana, mwaminifu, na tayari wakati wote, ni ujuzi na si wa kawaida.
- Uwajibikaji wa kitaalamu unamaanisha kukiri makosa yako, wala sio kudhibiti hisia za wengine. Hii ni kweli kwa kila ngazi la shirika.
- Heshima kwa wenzako, magari yao, ratiba zao, wakati wao, ndio inayofanya mahali pa kazi kua pazuri siku baada ya nyingine.
- Pangia kustaafu mapema. Pensheni si mshahara. Rekebisha matarajio yako mapema, hapo ndivyo maisha yako baada ya kustaafu yatakavyokuwa mazuri.